# OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA

SHULE YA SEKONDARI GALIJEMBE
S.L.P 599,
**MBEYA.**
08-12-2020,

PHONE NO:0762399856/0652312545

KUMB NA.GSS/S.5123/J.I/3.

JINA LA MWANAFUNZI …………………………………………

S.L.P ………………

**<u>YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI GALIJEMBE ILIYOPO WILAYA YA MBEYA MKOANI MBEYA KWA MWAKA 2021</u>**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Galijembe mwaka 2021, shule ipo umbali wa KM 17 kutoka stendi ya mabasi nanenane.

Usafiri wa mabasi kutoka nanenane unapatikana kwa Tsh.1500/=. Muhula wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 10/01/2021. Na mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe 19/01/2021. Muda wa kuripoti ni kuanzia saa 2:00 asubuhi mpaka saa 10:30 jioni baada ya hapo mwanafunzi hatapokelewa.

## 2.1 SARE ZA SHULE

A. Sketi mbili (2) moja dark blue na nyingine nyekundu iliyokolea, mshono wa sketi ni rinda box mbele na nyuma na ndefu sana, kitambaa kimeambatanishwa kwenye fomu. Zingatia rangi na aina ya kitambaa kilichoambatanishwa.

B. Mashati mawili (2) meupe yenye mikono mifupi.

C. Masweta mawili (2) rangi ya damu ya mzee.

D. Soksi nyeupe jozi mbili (2).

E. Viatu jozi mbili (2) vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi, vya kufunika miguu vyenye kamba, jozi moja ya ndala kwa ajili ya kuogea.

F. Jozi (pea) moja ya viatu vya wazi (sandal) visivyo na kisigino kirefu.

G. Kwa wanafunzi wa kislamu Hijabu ni nyeupe isiyokuwa na urembo.

H. T.shirt moja ya rangi ya light blue yenye kola na mistari myeupe shingoni na mikononi.

I. Magauni mawili (2) ya light blue kwa ajili ya kushindia, kitambaa cha satini mshono ni solo ndefu.

**2.2 KUTOKANA NA WARAKA WA ELIMU NAMBA 6 WA MWAKA 2015 KUHUSU UTEKELEZAJI WA ELIMU MSINGI BILA MALIPO MZAZI/MLEZI ATAKUWA NA MAJUKUMU YAFUATAYO:-**

a) Kununua sare za shule na michezo vifaa vya kujifunzia vikiwemo madaftari, kalamu pamoja na chakula.
b) Kugharamia matibabu kwa watoto wao.
c) Kulipia nauli ya kwenda na kurudi nyumbani wakati wa likizo.
d) Kununua magodoro, shuka, vifaa vya usafi binafsi kwa wanafunzi.
e) Kukemea na kutoa taarifa kuhusu mienendo inayokwenda kinyume na elimu msingi bila malipo, kwa kuwa Galijembe sekondari ni shule ya hostel gharama za chakula na hostel zimeambatanishwa na barua hii.

**2.3 VIFAA VYA MADARASANI**

a) Madaftari kumi (10) Counter Book 3 Quire
b) Kalamu za wino na risasi za kutosha (pen na pencil)
c) Mkebe ( mathematical set) na mathematical table (four figure)
d) Kamusi ya kiingereza (dictionary English – English)
e) Daftari ndogo tisa (9) kwa ajili ya mazoezi.
f) Karatasi nyeupe kwa ajili ya mazoezi (ream paper 01).
g) Graph paper moja.
h) Fail moja.

**2.4 MAHITAJI BINAFSI YA BWENI**

a) Blanketi zito, mashuka pea (2) moja rangi ya pink na light blue.
b) Mto na foroja ya pink na light blue
c) Ndoo (2) kwa ajili ya kufulia na kuogea
d) Sanduku la chuma lenye kufuli (tranker)
e) Kanga (2) mbili au vitenge au taulo kwa ajili ya kuogea.
f) Godoro futi 2.5x6
g) Picha nne za passport size za rangi za kitambaa cha blue.
h) Mwamvuli mmoja
i) Cheti cha kuzaliwa au uthubitisho wowote wa uraia.
j) Sahani ya draft (vyumba) kijiko kikombe
k) Aje na taulo za kike (pad) bunda 3.
l) Sabuni, mafuta, mswaki na dawa ya meno, kitana, dawa ya viatu nyeusi na brash ya kung'arisha viatu.

**2.5 CHAKULA**

a) Mwanafunzi anatakiwa kula chakula kinachotolewa na shule, shule haitoi chakula maalumu, mwanafunzi haruhusiwi kujipikia au kuwa na chakula cha nyumbani.
b) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na vyakula shuleni.

**2.6 VIFAA VYA MICHEZO**

a) Tracksuit (1) rangi nyeusi (adidas) yenye ufito mweupe.
b) Raba na socks za michezo (socks rangi nyeusi).

**2.7 VIFAA VYA KAZI NA USAFI**

a) Mopa (1) na brash ngumu (hard broom) moja (1) yenye mshikio mrefu.
b) Fagio mbili za chelewa.
c) Jembe moja (1) lenye mpini na fyekeo (kwanja).

## 3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule nzima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya joini (preparations.)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hivyo wakati wote wa uanafunzi wako.
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.

**NB:- Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele.**

g ) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
h ) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i )Kutunza mali za umma.

**3.1 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE AU KUSIMAMISHWA SHULE.**

a) Uwizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kuberi nk.
d) Ubakaji
e) Kupigana na kupiga.
f) Kuharibu makusudi mali ya umma.
g) Kudharau bendera ya taifa
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki, kuvuruga amani na usalama wa watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kutoroka shule au kulala nje ya shule bila ruhusa
n) Kutokuwepo shuleni bila ruhusa kwa muda wa siku 30 mfululizo.
o) Kumiliki simu

**4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mikataba ya kutoshiriki migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

**5.0 KUTOKA NJE YA SHULE**

Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa shule.

**6.0 AFYA ZA MWANAFUNZI**

a) Huduma ya kwanza hutolewa shuleni kabla ya mgonjwa kupelekwa hospitali kwa matibabu zaidi.
b) Tunaomba mzazi /mlezi uwe muwazi katika kutoa taarifa ya mtoto wako kuhusu hali halisi ya afya yake. Ikiwezekana vyeti vya matatizo ya kiafya kutoka kwa daktari vikabidhiwe kwa mkuu wa shule ili apewe huduma sahihi tatizo linapojitokeza akiwa shuleni.
c) Ni muhimu mwanafunzi awe na bima ya afya na aje nayo na kukabidhi kwa mkuu wa shule ili imsaidie kwa matibabu ya ngazi ya juu ya shule. Mwanafunzi asiye na bima ya afya aje na Tsh.6000/= ili aweze kukatiwa bima ya afya ya jamii atakayotumia kwa mwaka mmoja (1)
d) Mwanafunzi haruhusiwi kutunza dawa bwenini.
e) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na dawa za mitishamba shuleni.

**NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA NA KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA GALIJEMBE.**

**…………………….**
**ANNA M. PASCAL**
**MKUU WA SHULE**

**MCHANGANUO WA GHARAMA ZA CHAKULA KWA KILA MWANAFUNZI.**

| S/N | AINA YA CHAKULA | KIASI KWA MWANAFUNZI 1 KWA MLO | KWA SIKU | KWA WIKI | KWA MWEZI 1 | KWA MWAKA | TSH. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MCHELE | 0.25Kg | 0.25 | Mara 2=0.5Kg | 2Kg | 20Kg | @1,950/=39,000/= |
| 2 | MAKANDE | 0.25Kg | 0.25Kg | Mara 3=0.75Kg | 3Kg | 30Kg | @1,000/=30,000/= |
| 3 | MAHARAGE | 0.125Kg | 0.25Kg | Mara 14=2Kg | 8Kg | 78Kg | @1,900/=148,200/= |
| 4 | UNGA ( Ugali+Uji) | 0.276Kg | 0.5Kg | Mara 9=2.265 | 9Kg | 90Kg+7Kg=97 Kg | @1,500/=145.500/= |
| 5 | NYAMA | 0.125Kg | 0.125Kg | 0.125Kg | 0.5Kg | 5 Kg | @5,000/=25,000/= |
| 6 | SUKARI | 50Gm | 50Gm | 350Gm | 1.5Kg | 15Kg | @2,500/=37,500/= |
| 7 | MAFUTA | 0.0068 lita | | 0.0476 | 0.19 Lita | 2 Lita | @3,800/=7,600/= |
| 7 | CHUMVI | 0.0051Kg | Mara 2 0.0102Kg | Mara 70.036 | 0.4Kg | 1.5Kg | @1,000/=1,500/= |
| 8 | KUNI | | | 2.9 | 11.6 | 116@=690 | 80,040/= |
| 9 | MBOGA ZA MAJANI | ¼ ya fungu @1=400/= | 100/= | Mara 2 200 | Mara 8 800/= | Mara 80 8,000/= | 8,000/= |
| 10 | MATUNDA | | | Mara 1 100 | Mara 4 400 | 4000/= | 4,000/= |
| 11 | VITUNGUU | 1 | | Mara 28.5/= | 17/= | 170/= | 170/= |
| 12 | NYANYA | | | 17 | 34 | 340/= | 340/= |
| | **JUMLA** | | | | | | **526,850/=** |

**2. MCHANGANUO WA GHARAMA ZA HOSTELI KWA KILA MWANAFUNZI**

- Malipo ya watumishi ………………34,800/=
- Umeme …………………………….. 8,000/=
- Matibabu ……………………………10,000/=
- Mfumo wa maji taka …………………3,300/=
- Vifaa vya jikoni ………………………3,690/=
- Ukarabati …………………………....3,800/=
- Mawasiliano …………………………..1,700/=

**JUMLA KUU (chakula na gharama za hosteli)………………….592,200/=**

**Fedha zitalipwa kwa awamu nne kama ifuatavyo:-**

- Awamu ya kwanza January 200,000/=
- Awamu ya pili March 100,000/=
- Awamu ya tatu July 200,000/=
- Awamu ya nne September 92,200/=

**AKAUNTI NAMBA**
**61010036195 BENKI YA NMB.**
**JINA LA AKAUNTI: GALIJEMBE GIRLS' SECONDARY SCHOOL**
**NB: Mwanafunzi hatapokelewa bila ya pay in slip.**

## TAARIFA BINAFSI

1. Jina kamili la mwanafunzi …………………………..

2. Jina kamili la mzazi ……………………………

   Anwani kamili …………………………….

   ……………………………….

   Namba ya simu ………………………………

   Mkoa ………………………………………

3. Majina ya watu watatu ambao mawasiliano ya kiofisi kuhusu mwanafunzi yatafanyika

| JINA | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|
| 1) ……………………… | ……………. | …………………… |
| 2) ……………………… | …………… | …………………….. |
| 3) ……………………… | ……………. | …………………….. |

4. Jina na sahihi ya mzazi/mlezi

   Jina …………………………………………………….. sahihi ……………

5. Jina kamili la Afisa Mtendaji

   Jina …………………………………………………….. sahihi ……………

6. Taarifa hii irudishwe kwa Mkuu wa shule ya Sekondari Galijembe

**……………………**
**ANNA M. PASCAL**
**MKUU WA SHULE**

ANUANI YA MZAZI /MLEZI
…………………………………
……………………………………
……………………………………
Tarehe ………………………….

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI GALIJEMBE,
S.L.P 599,
**MBEYA.**

**YAH: HATI YA KUKUBALI MASHARTI KUHUSU MTOTO WANGU KUSOMA SEKONDARI YA GALIJEMBE.**

Mimi …………………………………………….. Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi ………………………………… Aliyekuwa akisoma shule ya msingi ……...………. Katika Wilaya ya …………………………………….

Ninakubali mtoto wangu asome shule ya sekondari Galijembe iliyopo Wilaya ya Mbeya kwa kufuata masharti yafuatayo:-

1. Kwamba mtoto wangu atahudhuria masomo kama kawaida na kufanya shughuli nyingine zote za shule tangu kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne, na atazingatia sheria na taratibu zote za shule.
2. Nakubali masharti na gharama zilizotolewa katika barua ya kuitwa kwa mwanafunzi (*Joining Instructions*) na nitayatimiza kwa wakati unaotakiwa.
3. Nitahakikisha atafika kwa kufuata tarehe iliyopangwa kwa kipindi chote cha miaka minne.

……………………….
TAREHE

… ………………………
SAINI YA MZAZI/MLEZI

**MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKAMIGOMO  FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

Mimi …………………………………………………. Mwanafunzi wa shule ya sekondari Galijembe ninakiri kwamba sitashiriki katika migomo, fujo na makosa yote ya jinai muda wote nitakaokuwepo hapa shuleni. Endapo imethibitika kuwa nimefanya makosa hayo hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yangu.

……………………………….

Saini ya mwanafunzi

**JINA LA MWALIMU WA NIDHAMU…………………………………………….**

**SAINI ………………………………..……**

**MKUU WA SHULE ……………………………………………..**

**SAINI ………………………………………………..**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE AND TECHNOLOGY**

**GALIJEMBE SECONDARY SCHOOL,**
**P.O. BOX 599,**
**MBEYA.**

**TO.**
**MEDICAL OFFICER,**
**………………………..**
**………………………..**
**……………………….**
**Please examine**
**……………………………………………………………………………..**
As to her fitness for pursuing further education in this school

1. Hemoglobin ……………………………………………………………
2. P.v Bleeding ……………………………………………………………
3. Sight ……………………………………………………………………
4. Blood pressure …………………………………………………………….
5. Urine of sugar and pregnancy test ……………………………………..
6. Stool routine examination …………………………………………….
7. Asthma ……………………………………………………………….
8. Skin disease ………………………………………………………….
9. Leprosy ……………………………………………………………….
10. Epilepsy ……………………………………………………………….
11. Pulmonary tuberculosis ……………………………………………
12. Deformity ……………………………………………………………
13. Mental problem ……………………………………………………
14. Comments ……………………………………………………………

Sign …………………………..
Official stamp